

AL SIRATUF MUSTAQIIM

Watu mia moja na nne, waume, wanawake na watoto walipanda ndege aina ya MI 185 tarehe 19 Desemba 1997 kutoka Jakarta.

Wakati ndege ilipokuwa ikinapaa kuelekea Singapore, hakuna hata mmoja wao aliyeweza kujuu kuwa hawatafika mwisho wa safari yao. Ndege yao Boeing 737 aina ya Jeti ghafla karibu na Palembong ilipiga mbizi na kupasuka vipande vipande karibu na Sungai Musi, na kuua abiria wote pamoja na wafanyikazi wote wa ndege hiyo.

Watu wote duniani wanapata majanga makubwa ya vifo, matetemeko ya ardhi, vimbunga, ajali mbali mbali. Hayo ni mifano ya majanga yanayo kuja ghafla bila kutegemea, hivyo watu wanakuwa hawana uwezo wa kudhibiti vifo vya namna hiyo.

Watu wengine wanakufa kutokana na magonjwa yasiyotibika. Kila mmoja wetu anajaribu kujitayarisha kwa ajili ya kifo, lakini kifo siku zote hakitabiriki na hakidhibitiwi.

Baadhi ya watu wanajaribu kuishi maisha marefu kwa kutovuta sigara na kufanya mazoezi ya viungo, kula vyakula bora, pamoja na kunywa vidonge vyenye kuongeza afya (vitamini). Pamoja na hayo, hatuwezi kukataa ukweli kuwa siku moja tutakufa.

Watu wengine hawafikirii kuhusu kifo, wakati wanapokuwa hawakabiliwi na matatizo, wakati wanapokuwa na uwezo wa kuwa na chakula na fedha, wakati hakuna matatizo ya kifamilia na wanapokuwa na nafasi/ cheo katika jamii, kifo kinakuwa mbali na mawazo yao. Lakini kifo hakifiki kwa watu wazee na wenye shida tu, pia watu wenye akili na vijana wanaweza kufa bila taarifa. Kifo kinaleta usawa kwa wote tokia tabaka kwa juu hadi tabaka ya chini.

Mungu, ana madaraka ya kutuweka mbinguni na kutuhukumu jehanamu kulingana na hukumu yake. Jina lake Ar Rahmani Rahim [yeye Masiha na mkamilifu] hivyo anatuonya tujihadhari na kujitayarisha wakati wote kwa kifo na kiama . Kila mtu atakufa siku mmoja na badaye kuhukumiwa siku ya hukumu, wakati kila moja atahukumiwa kutokana na matendo yake aliofanya wakati wa maisha yake duniani

Hivyo Mungu anatutaka, tuwe tayari muda wote kuanzia sasa. Aliye tayari wakati wowote ni yule anaye tembeya katika njia iliyo nyofu katika amani ambayo Mungu pekee ndiye anatoa.

DUNIA HII NI YA MUDA

Nini maana ya maisha haya?

Dunia ni ya muda mfupi. Uhai huu, na hata utajiri wa dunia ni kama mvuke unaonekana kwa muda mfupi na kutoweka na kuyeyuka. Lakini maisha yetu katika dunia hii ni marefu kuliko dunia hii ambayo tumepewa na Mungu anayeishi milele.

Watu wengi wanaamgalia furaha ya maisha katika dunia hii tu. Kila siku tunashughulikia mipango ya dunia hii tu. Shughuli nyingi za kutafuta fedha, kufanya kazi, na kufurahia vivutio ambavyo vinatoweka baada ya mda mfupi. Tunaona kuwa pilka pilka hizi zote zinaisha na kupoteza maana ya maisha.

Shetani pia anakazana kutushawishi kuenenda katika furaha hii ambayo si rahisi. Anatutaka tupoteze maisha kwa kutufanya tutende dhambi ili tuwe wakazi wake milele.

Mara nyingi. Ni kweli kuwa taabu tunayopata katika dunia hii ni kubwa kuliko furaha tuliyonayo. Tunasahau kuwa sisi sote tutatakiwa turudi kwa Mungu ambaye ndiye mwenye uhai wetu. Tunasononeka na kupoteza maana ya maisha.

Lakini Mungu siku zote anatupatia mwongozo wa kuona furaha ya kweli ni lipi. Tunapokuwa tunafuata mwongozo wake, tunapata nguvu za kujiongoza wenyewe katika njia hiyo kutoka kwake Bwana na hivyo ambako hakuna dhambi.

Maisha baada ya hapa kuna njia mbili katika roho ya binadamu; Mbinguni na Jehanamu. Mara Roho mtakatifu atakapo tuhukumu siku ya hukumu, na kuingia aidha katika moja ya njia hizi, hatutaweza kupona au kubadili uamuzi wa njia / hukumu, na tutaishi katika njia hiyo milele.

Kwa vile hatuwezi kujua ni lipi tutafuata, sasa ni nafasi yetu kuchagua mwelekeo wa maisha yetu ya baadaye.

Ni maisha yapi ya baadaye unayachagua?

MBINGUNI

Mbinguni ni mahali pazuri sana, na pa kuishi milele. Mbinguni kumejaa na hewa baridi, mbuga nzuri zenye sauti zenye salamu za amani na kuzungukwa na hewa safi na mbuga za kuvutia zenye sauti ya amani iliyojaa upendo na heshima.

Mawazo ya binadamu hayawezi kuelezea kikamilifu uzuri wa mbinguni. Maandiko yanayoonyesha kuwa waumini waliojazwa na ufufuo wa milele katika Mungu wako huru kutoka katika maovu ya dhambi. Furaha kubwa iliyojaa na kumtukuza daima mwenyezi Mungu ambaye ametuondolea masikitiko na majonzi milele.

Ni kwa njinsi gani sisi tulio waovu waume kwa wanawake tunaweza kuwa na furaha hiyo? Ni wale tu ambao wametukuzwa na Baba Mungu ndio wataingia mbinguni. Katika Alquarim Alqarim, mwenyezi Mungu anatufunulia kuwa alimchagua Isa Al Masih Aleisalam mwana wa Mariam kuwa zawadi ya ufufuo kwa kila mwanadamu.

Mbinguni na Duniani, mwenyezi Mungu ameteua jina la Isa Aleisalam Masiha aliyetabiriwa kuwa pekee mbinguni na duniani.

“— yeye aliye na jina la masiha ni kielekezo duniani na kwengineko”.

KUZIMU

Kuzimu ni sehemu / mahali panapotisha sana. Wale waishio huko wanapata taabu sana kwa sababu mavazi, mamblanketi na vitanda vyao vimetengenezwa kwa moto. Juu ya vichwa na chini ya miguu yao kila mahali hapo kumeja na moto, moshi mweusi na giza kuu. Macho yao hayaoni, masikio yao hayasikii na midomo yao imekuwa bubu katika mahali hapo pa masikitiko. Pamoja na mateso makuu, mioyo yao haifi. “*Huzuni kuu imewajaa*” hata hivyo mioyo yao hapa haina matumaini ya wokovu. *Wakiwa hai, pia mioyo yao iko kama imekufa. Hakuna mwisho wa maumivu yao, maumivu ni ya milele.*

Tangu binadamu wa kwanza, Mtume Adamu, watu wote wameanguka katika majaribu ya dhambi. Wamekuwa wakitenda dhambi na hivyo kuadhibiwa katika kuzimu yenye mateso makubwa.

“*Na hakuna yeyote kati yenu bali kwenda kwake. Hii ni ahadi ya Bwana Mungu isiyoeupukika.*”

NJIA NYOOFU YA KWENDA **MBINGUNI**

Sisi sote tunajua kuwa ni wale tu wamwaminiyo katika Bwana ndiyo walio katika njia nyoofo ya kwenda Mbinguni.

Pia waumini wanaoenenda / wanaotenda kulingana na maombi na Bwana ndio watakaopata zawadi ya milele mbinguni.

Lakini ni wangapi kati yetu tunajua alama sahihi ambazo Mungu alitufunulia kwetu kuzifuata? Bila ya alama hizi kutoka kwa Mungu tunawezaje kuona njia iliyo nyoofo ya Mbinguni? Bila ya kujua njia zilizofunuliwa na Mungu, tutaweza kuongozwa naye na kuwa wafuasi wake.

Je kuna kiwango cha kiasi kinachotosha kwetu kuweza kuingia Mbinguni?. Ni kiasi gani tunatakiwa kutii barabara sheria za kanisa la Mungu kabla ya kuingia Mbinguni? Ni kwa kiasi gani maombi yanatosheleza kutufanya tuwe na uhakika wa kuingia Mbinguni.

Maelekezo ya namna ya kutunza dini hayajatoa jibu la kweli/wazi kwetu.

Pia, ni wangapi kati yetu wanaweza kutunza viwango vya mwenyezi Mungu kwa ajili ya kuingia Mbinguni?

Ni wangapi kati yetu tuna nguvu, upendo na ukamilifu wa kupita viwango vya utiifu na kutoa kunakotakiwa kabla ya kuingia mbinguni?.

Kwa matokeo hayo, watu wengi wako katika masikitiko makubwa, mashaka na wasiwasi hata kama wanasali ipasavyo na kutoa sadaka. Kwa miaka mingi (miongo mingi) Bwana Mungu ametuonyesha ni lazima tuombe kwake ili atuonyeshe njia ambayo yeye ametutayarishia.

“Tuonyeshe njia ilio nyooofu”

“Lo, Waumini wa kweli wanamuogopa mwenyezi Mungu na wanatafuta njia inayowaongoza kwenda kwake?.

Je unaijua njia hii?

MWENYE HURUMA NA UPENDO

Sababu Mungu ni mwenye “ huruma na upendo, yeye ametukumbusha na kutuhakikishia mwongozo wake wa namna ya kuingia Mbinguni. Na tusome Biblia kama yasemavyo hapa chini:

MWONGOZO KATIKA BIBLIA TAKATIFU NA ALHADITHI UNAMUWEZESHA MWANADAMU KUINGIA MBINGUNI

1. Isa Al Masih Aleisalam ni njia iliyonyoofu kufuatwa

“ Na Isa Aleisalam atakuwa alama (kwa ajili ya kuja) saa (ya hukumu): Hivyo usiwe na wasiwasi juu ya (wakati) bali nifuate Mimi. Hii ndiyo njia ilio nyooofu”

2. Isa Aleisalam ni mwanga wa kuabudiwa

“Wakati Isa Aleisalam alipokuja katika njia ilizo wazi, Alisema hivi: sasa ninakuja kwenu nikiwa na “ hekima “ kwa ajili ya kuweka wazi mambo yaliyo na utatanishi: mwogope Mungu na kumtukuza”

3. Isa Al Masih Aleisalam ananena neno la kweli juu ya mambo yaliyo na utatanishi. “Hivyo (yeye) Isa Al Masih Aleisalam mwana wa Mariamu (imekuwa) usemi uliyo wa kweli kwao wao (dhahiri) wanaupinga/wanakataa

4. Isa Al Masih Aleisalam ndiyo mtume wa Mungu na Neno.

“Isa Al Masih Aleisalam mwana wa Mariamu alikuwa mtume wa Mungu na neno lake”

5. Isa Al Masih Aleisalam, Roho Mtakatifu na Neno.

“Isa Al Masih Aleisalam alikuwa Roho wa Mungu na Neno”

6. Isa Al Masih Aleisalam ni “*IMAM MAHDI*” pekee.

(Mwongozo usioingilika) isipokuwa Isa Al Masih Aleisalam mwana wa Mariamu.

7. Isa Al Masih Aleisalam alizaliwa sio kwa matakwa ya Binadamu bali kutokana na Roho wa Mungu.

“Pia (kumbuka) mwanamke aliye ilinda utu wake : Tunaishi katika yeye aliye Roho na tunamweka yeye na Mwanaye kuwa allama kwa watu wote”

8. Isa Al Masih Aleisalam alizaliwa akafa na akafufuka

“Hiyo amani ipo juu yangu tangu nilipo zaliwa, siku nitakapokufa hadi nitakaponyakuliwa Mbiguni katika maisha ya milele (Mapya)”

9. Isa Al Masih Aleisalam aliy kuja, alitukuzwa na wafuasi wake wamepewa thawabu mbinguni.

“Angalia, Mungu anasema, Isa Al Masih Aleisalam atawachukua na kupaa nanyi kwangu na kuwaondolea (yatokanayo na machafu) wote wale wanaomtusi Mungu; Mtawaweka wale wote wanaomfuata kuwa mashujaa wa kuacha dhambi siku ya ufufuo.”

10. Isa Al Masih Aleisalam aliponya viwete na vipovu

“...Ninaponya waliozaliwa vipofu na viwete na nina wafufua wafu kwa njia ya bwana Mungu”.

11. Isa Al Masih Aleisalam alirundia kifo

“...angalia nakuja haraka katika wafu , kwa njia ya Bwana Mungu”.

12. Isa Al Masih Aleisalam alipewa miujiza na Roho Mtakatifu.

“kwake Isa Aleisalam mwana wa Mariam ,tunatoa alama iliyo wazi na kujiimarisha kwake na Roho Mtakatifu.”

13. Bwana Mungu anawachukulia wale wote wanaomkataa Isa Al Masih Aleisalam mtume wa.

Mungu kuwa wamelaaniwa.

“Kuwa wale wanaokataa ukweli , kuwa wanapinga Mariamu na ni “ mashahidi wa uwongo;”

14. Maandiko yote yanazungumza ukweli juu ya Isa Aleisalam Kritso.

"Na hakuna mwanadamu katika kitabu kitakatifu bali ni lazima kumuamini yeye kabla ya kifo chake na siku ya hukumu atakuwa shahidi juu yao."

15. Wale wote wanao kataa kitabu cha sheria ya Mungu (Torati) na injili, wanahasabiwa kuwa hawana dini.(makafiri).

"Sema; watu wa kitabu cha Mungu hamna sababu ya kusimama isipokuwa kusimama katika sheria ,neno la injili na ufunuo wote unaokuja kwenu kutoka kwa Baba Mungu ."

16. Isa Al Masih Aleisalam, neno la Mungu inakuja kutoka katika ufunuo wa Mungu kutufunulia kwetu maana ya kitabu cha Mungu.

"na kweli,... kwa hekima."

17. Isa Al Masih Aleisalam ana mamlaka /ufufo wa dunia na mbingu.

"Angalia , malaika wa Mungu asema; Mariamu Mungu amekupatia neno la upendo kutoka kwake ; Jina lake ataitwa Isa Al Masih Aleisalam ,mwana wa Mariamu kwa heshima yake katika dunia hii, na baadaye na kwa walio karibu na Bwana Mungu.

Bwana Mungu amempatia Isa Al Masih Aleisalam mamlaka na utawala wote juu ya dunia hii na ijayo. Isa Al Masih Aleisalam njia iliyo nyoofo. Tuna kumbushwa kataka Bibilia pale ambapo wafuasi wake Isa Aleisalam wamepewa tuzo mbingu Isa Al Masih Aleisalam alikuwa muhimu kwa Mungu hivyo jina Isa Aleisalam lime tajwa mara 97 katika Bibilia.

Mbingu zinaweza kulinganishwa na (ikulu) au makao makuu ya nchi. Kama Rais wa nchi atakualika katika Ikulu, utakuwa na uhakika kuwa utaingia Ikulu kwa sababu aliye kualika ndiye mwenye mamlaka yote na anamandaraka yote ya Ikulu.

Hata hivyo, iwapo waziri ambaye ana mamlaka juu ya sehemu yeoyote ya Ikulu atakualika uende Ikulu,ni wazi utasita kwa sababu inawezekana ukatumia fedha minge na usiruhusiwe kuingia.

Kwa neema,Mungu kama Rais wa nchi amemchagua Isa Al Masih Aleisalam, kuwa Roho na alama kwa binadamu kwa ajili ya kutuokoa kwenda mbinguni. Isa Al Masih Aleisalam amekuja kutoka sehemu ilyo karibu sana na Mungu,kutuletea mwaliko huu wa neema toka kwa Mungu ukiwa na mamlaka timilifu.

Kwa sababu Isa Al Masih Aleisalam alikuja kwa njia ya neno la Mngu kutoka katika kitabu kitakatifu.Mbinguni, neno lake halina uongo, na hana dhambi.Kwa vile neno la Mungu ni lazima ufanjike/lifanikiwe, ametimiza ujumbe wa wokovu wa Mungu kikamilifu, wale wote wanaopata ujumbe huu na kumfuata yeye aliye njia nyoofo ya Mungu,wataishi katika neema na kuingia mbinguni hakika.

Tangu Bwana alipoazimia hapo **Alquran Alqarim** kuwa Bwana amepewa tuzo kuwa hapa duniani na mbinguni,wale wote wanaofuata maelezo yake watapata dhawabu mbinguni. Mfalme Mohamed aliwasilisha ujumbe huu kwetu pale **Alquran Alqurim** na Alhadith kutoka katika ufunuo wa kifo chake.

RAFIKI WA KWELI

Maombi ya Mtume Muhammed kabla ya kifo chake:

“Ee Mungu wangu, nisamehe nionee huruma na uniunagnishe na Rafiki wa Kweli”

Basi Mtume Muhammed akainua mikono juu na kusema

“Ewe rafiki wa Kweli”

Basi akaiweka mikono yake chini akafa.

Je huyu rafiki wa kweli ni nani?

Kulingana na kisanga cha Hadith, hawa marafiki wa kweli wanaweza kuwa “Malaika” au “Wanabii”. Lakini Malaika hawajulikani kama marafiki wa Kweli. Kwa hivyo rafiki wa Mtume Muhammed hawakuwa Malaika bali Nabii.

Kati ya wanabii ambao wanaweza kutambuliwa kama Rafiki wa Kweli ni nani?

“Adam Shafiullah”

“Nuh Najiyullah”

“Ibrahim Khalilullah”

“Ismail Dzabihullah”

“Musa Kalimullah”

“Dawud Khalifullah”

Lakini yeye mwenyewe asema

“Mwenye neema na mwenye huruma”

“Niko karibu na Isa Aleisalam Mwana wa Mariam duniani na Mbinguni. Manabii wote wana husiana kwa sababu ya jamii moja. Mama wanaweza kuwa tofauti lakini dini ni moja”.

“...Isa Aleisalam Mwana wa Mariam aheshimiwa duniani kote na baadaye. Na wale walio karibu na Allah.

“Kuapa kwa Allah, kwani moyo wangu umkononi mwake.kwa maana wakati umekaribia usiku ambapo mwana wa Mariamu ashuka kati yenu. Atakuwa hakimu mtakatifu.”

“Hakuna Imam Mahdi ispokuwa Isa Aleisalam mwana wa Mariamu”

“...Isa ni Roho wa Allah, mtumwa wa Mungu na neno la Mungu.”

Kwahivyo rafiki wa kweli ni Isa mwana wa Mariamu.Rafiki wa kweli alitumwa na Allah kuja kusema hivi

“...Mtii hii ni njia nyooofu.”

“...Bali msiwe kama wale wanaosema, Tunasikia lakini hatusikizi: Kwa mabaya ya mnyama mbele ya Allah ni visiwi na wasio zungumza na wasio elewa.”

RAFIKI WA KWELI ATUSAIDIA VIPI LEO?

1) Thibitisho wa Rafiki wa kweli inaonyesha wazi Siratul Mustaqiim

“Kwa Isa Aleisalam mwana wa Mariamu tulipeana nakala na kumtia nguvu kwa Roho Mtakatifu... Na kusiwe na rehema kwa dini: Ukweli wasimama kutoa makosa”

Pengine kwa dini yetu tulifuata njia za kitamaduni kuliko njia za miujiza za Allah. Tuna weza kuwa tumekosea yale Mtume Mohammed alielewa. Sote tunahitaji miujiza kamili kutoka kwa Mungu kupitia kwa Rafiki wa Kweli! Na tuache njia ye yeyote ambayo haipatikani katika kitabu cha Allah.

Ishara zake zinanyesha ya kwamba uongo wa Shoitan::Zina onyesha njia za ukweli za Allah.

Wale walioziacha njia zingine ili kufuata ishara za Isa Aleisalam wanafuata mwelekezo wa neema ya Mungu..Wako tayari kwa kifo na hukumu.Tuna uhakika wa ndani wa kuingia mbinguni kwa sababu walichukua kimbilioa la haki kwa rafiki wa kweli.Wako huru kwa hukumu yoyote kwa sababu hawategemei mtu ye yeyote wala hawategemei mazuri yao wenyewe.

Ewe Al Mu'mineen, usipuuze hizi ishara za Kalimatullah Isa.Tii na utaona Siratul Mustaqiim ikithibitishwa maishani mwako.

JE TUMEPUUZA NJIA ZINGINE?

Je tumeongozwa na maneno ya kimiujiza ya tulioyopewa na rafiki wa kweli kutoka kwa Allah?

2) Rafiki wa kweli anatusaidia sasa kwa kushikilia na kutushikilia anatusaidia kuelewa Siratul Mustaqiim

Allah ambaye hatuwezi kumguza amesongesha mkono wa imani kwetu sote katika dunia hii kwa njia nzuri ambayo sisi wenyewe hatuwezi kuelewa.

“...Yeyote.. amwaminio Allah amejinyakulia utajiri wa dhamana mkononi usio vunjika.”

Hii Ayat ul Kursi inaonyesha wazi tukitazama katika aya ya 253: Tuna usalama tukiamini katika ishara ya Yeus na Mitume.

- O Usalama kama huo kutoka kwa Allah inatoka kwenye mkononi mwake. Ni katika utakatifu huu tunaweza kuwasiliana na Allah, yeye pekee, na hata Roho kwa Roho.
- O Ni yeye pekee ndiye tunaeweza kumwamini kwa sababu yeye ndiye wa kweli kikamilifu.
- O Usalama wake haivunjiki kwa sababu alijaribiwa kikamilifu na aliquwa na amani

hata wakati wa matatizo ya dunia hii kwa binadamu.

Kwa hivyo amani ilikuwa na mimi wakati nilipozaliwa, wakati nilipo kufa na wakati nitakapofufuka tena.

MKONO MWANINIFU AMBALO **HALIVUNJIKI**

Katika maisha na kifo, tunaweza kuwa na amani ya milele tukiamini katika miujiza ya Allah kuhusu maisha na kifo.

Hata Mtume Muhammed Al Mustafa hukutegemea katika Jihad yake mwenyewe and akatumaini kwa usalama ya Yule Rafiki wa Kweli alipo kuwa akiondoka Ulimwenguni huu.

Je, tunawezaje kulia zaidi kwa imani hata sisi?

**Je, tunausalama katika mkono usiovunjika wa Rafiki wa Kweli,
Isa Aleisalam ambaye ni Mtume maalum wa Allah?**

Allah akubariki na nguvu zake katika Siratuf Mustaqiim.